# HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO MHE. PASCAL KIHANGA WAKATI WA KUWASILISHA RASMI BAJETI YA MWAKA 2017/2018 KATIKA KIKAO MAALUMU CHA BAJETI CHA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA TAREHE 12/01/2017

**Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Morogoro,**

**Mhe. Naibu Meya,**

**Waheshimiwa Wabunge,**

**Katibu Tawala Msaidizi Mkoa, Huduma za Serikali za Mitaa,**

**Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro,**

**Waheshimiwa Madiwani,**

**Mkurugenzi wa Manispaa,**

**Wakuu wa Idara na Vitengo,**

**Watendaji wote,**

**Ndugu Wananchi,**

**Wanahabari,**

**Wageni Waalikwa,**

**Mabibi na Mabwana.**

**Asalaam Aleykum!**

**Bwana Yesu Asifiwe!**

Awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote kufikia mwaka 2017 tukiwa na afya njema wote na kuwa hapa leo hii, pia nawakaribisha Wananchi wote mliohudhuria kikao hiki Maalumu cha kupitia na kupitisha mapendekezo ya mipango na bajeti 2017/2018.

Ninawashukuru Watendaji na Wadau wote wa Halmashauri walioshiriki kwa pamoja kwa namna moja au nyingine katika kukamilisha mchakato wa maandalizi ya bajeti hii hadi kufikia kiwango hiki ambapo leo itajadiliwa na kutolewa maamuzi rasmi.
Ninawashukuru sana Waheshimiwa Madiwani kwa maelekezo yenu ya msingi mliyoyatoa wakati wa kujadili bajeti hii kupitia Kamati zetu za Kudumu za Halmashauri.

Ninawashukuru Wananchi wote kupitia Mabaraza ya Maendeleo ya Kata na katika vikao vilivyofanyika katika nyakati na ngazi mbalimbali. Ninapenda kuwahakikishia kuwa mawazo yenu yamezingatiwa kwa kadiri ilivyowezekana katika maandalizi ya bajeti hii.

Aidha, ninawashukuru wote mliotenga muda wenu leo kuhudhuria kikao hiki muhimu. Kuwepo kwenu hapa ni kielelezo cha kutambua umuhimu mlioipa bajeti hii hususani umuhimu wa kujua hali ya utoaji wa huduma na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Manispaa yenu kwa mwaka 2017/2018.

Ninatambua na ninafurahi sana uwepo wa Waandishi wa habari hapa kwani kupitia kwenu taarifa zitaweza kuwafikia Wananchi ambao hawakuweza kuwa nasi hapa leo. Kwenu wote ninasema ahsanteni sana.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kupanga na kutekeleza Bajeti yetu ya mwaka 2017/2018.

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Kama mjuavyo, Halmashauri yetu huendeshwa kwa kuzingatia maelekezo ya ilani ya Chama Tawala, Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo mbalimbali ya Taifa chini ya usimamizi wa Baraza la Madiwani kupitia Kamati zetu za kudumu.

Kwa msingi huu na kwa kuzingatia Dira (vision) na Dhamira (Mission) ya Halmashauri ya kutoa huduma bora na endelevu Kiuchumi na Kijamii ili kufikia azma ya maisha bora kwa kila Mwananchi, ambapo Manispaa imepanga kutekeleza mipango mbalimbali ya Kitaifa na ile iliyobuniwa na Halmashauri yenyewe katika ngazi ya Mtaa,

Kata na ya Halmashauri kwa kuwasilisha rasimu ya mapendekezo ya bajeti hii ya mwaka 2017/2018 kwenye Baraza hili kwa lengo la kuichambua, kuijadili na hatimaye kuipitisha.

Ninapenda kulihakikishia Baraza hili kuwa, bajeti hii pamoja na mambo mengine, imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 – 2020 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Halmashauri yetu imepata mafanikio katika maeneo mbalimbali tangu mwaka 2010. Nichukue fursa hii kuelezea kwa uchache mafanikio, changamoto na mikakati yetu katika baadhi ya maeneo yafuatayo:

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

**(a) Kuhusu sekta ya Uchumi na Uwekezaji**:
Ili kuongeza kipato Manispaa kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za fedha inatarajia kujenga maeneo ya biashara ikianza na ujenzi wa Soko Kuu. Aidha mapitio ya uandaaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Soko kuu na taarifa ya tathimini za athari za kimazingira na kijamii zinaendelea. Kwa sasa Halmashauri inakamilisha nyaraka mbalimbali baada ya kusaini MOU na Uongozi wa Benki ya TIB ili iweze kupata mkopo kwa ajili ya ujenzi huo.

Halmashauri kwa kutumia fedha zake za ndani inagharamia kazi ya mapitio ya uandaaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu, uandaaji wa tathimini ya athari za kimazingira na kijamii,uandaaji wa mpango biashara wa soko, uandaaji wa michoro na gharama za ujenzi (BOQ) kwa ajili ya ujenzi wa Soko kuu hilo.

**(b) Kuhusu Sekta ya Miundombinu**:

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri iko kwenye hatua ya utoaji wa tunuku ya mikataba (Contract award) katika kazi zifuatazo;-

- Barabara za Kilombero (Kihonda) - Mazimbu Campus (1.05km), Kilakala (0.56km na barabara ya Sultani (0.42km) kwa kiwango cha lami

- Matengenezo kwenye sehemu korofi Barabara za Sabato, Forkland, Pangawe - Kingolwira, DSM - Mafisa, RusegwaII, Mgulasi Secondary School, VETA (Kihonda) – Kihonda – Tungi DSM, Misitu – Ngerengere -Msamvu, Fungafunga na barabara zinazozunguka Kituo cha mabasi cha Msamvu zenye urefu wa jumla ya km 29.14

- Matengenezo ya mara kwa mara kilomenta 431.47.

**(c) Kuhusu Sekta ya Ardhi**:

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Manispaa itaendelea kupima na kugawa viwanja **500** ili kuweka mji katika mpangilio mzuri na kuboresha mazingira kwa kushirikina na Benki ya Rasilimali Tazania ( Tanzania Investment Bank) .

Manispaa inaandaa mpango mpya wa kusimamia ukuaji wa mji yaani Mpango kabambe wa Manispaa ya Morogoro (The Morogoro Master Plan 2015 – 2035)kwa kushirikiana na sekta Binafsi na za Umma.

Aidha itaendelea kutekeleza mpango wa kuendeleza eneo la mji kati ya Biashara( Centre Businness District) ikiwa ni pamoja na mpango mkakati wa Maendeleo ya mji ( Strategic Urban Development Plan)2008-2028.

Sambamba na hilo Manispaa imeingia ubia wa uendelezaji wa shamba la mkonge la Tungi kwa kushirikiana na wamiliki wa shamba hilo Dominion Plantantions Limited wa Dar Es Salaam ili kujenga mji mpya wa Tungi (TUNGI SATELITE TOWN).

Mji huo mpya utawezesha Manispaa hii kufikia vigezo vya kuwa Jiji kutokana na huduma mbali mbali kama viwanda, biashara, utalii, Bandari ya Nchi kavu na Hospitali ya Rufaa ya Kanda.

**(d) Kuhusu Sekta ya Elimu ya Msingi**:

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Kwa mwaka **2014**, jumla ya Watahiniwa **5896** wakiwemo Wavulana **2740** na Wasichana **3156** walitegemewa kufanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Hata hivyo, jumla ya wanafunzi **5826** wakiwemo Wavulana **2707** na Wasichana **3119** sawa na **asilimia 98.0** walifanya mtihani huo. Aidha, jumla ya Wanafunzi **4356** wakiwemo Wavulana **2,337** na Wasichana **2378** sawa na **asilimia 75.6** walifaulu na kujiunga na Elimu ya Sekondari kwa **asilimia 100**.

Kwa mwaka **2015**, jumla ya Watahiniwa 6319 wakiwemo Wavulana 2967 na Wasichana 3352 walitegemewa kufanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 6250 wakiwemo Wavulana 2927 na Wasichana 3323 sawa na **asilimia 99.0** walifanya mtihani huo. Aidha, jumla ya Wanafunzi 4,771 wakiwemo Wavulana 2,529 na Wasichana 2,242 sawa na **asilimia 76** walifaulu na kujiunga na Elimu ya Sekondari kwa **asilimia 100**

Kwa mwaka **2016**, jumla ya Watahiniwa 6700 wakiwemo Wavulana 3236 na Wasichana 3464 walitegemewa kufanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 6660 wakiwemo Wavulana 3220 na Wasichana 3440 sawa na **asilimia 99.4** walifanya mtihani huo. Aidha, jumla ya Wanafunzi 5225 wakiwemo Wavulana 2,498 na Wasichana 2727 sawa na **asilimia 78** walifaulu na kujiunga na Elimu ya Sekondari kwa **asilimia 100**

### (e) Kuhusu Sekta ya Elimu ya Sekondari.

Halmashauri ina jumla ya shule 49, kati ya hizo 23 ni za Serikali na 26 ni binafsi. Jumla ya wanafunzi **5,177** walijiunga na shule za sekondari za Serikali hadi Januari 2017, kati ya hao wavulana ni **2,465** na wasichana ni **2,712**. Idadi ya walimu imeongezeka kutoka 823 mwaka 2013 hadi **1,299** mwaka 2016.

Kati ya hao **953** ni walimu wa masomo ya sanaa na **346** ni walimu wa masomo ya sayansi. Hivyo halmashauri ina zaida ya walimu wa sanaa **400**. Na upungufu wa walimu **37 wa masomo ya Hisabati na sayansi.**

### MIUNDOMBINU NA SAMANI

Kumekuwa na ongezeko la miundombinu ikiwemo madarasa, maabara za sayansi, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na samani katika shule za sekondari kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano madarasa yameongezeka kutoka 260 mwaka 2013 hadi 343 Desemba 2015, nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 44 mwaka 2013 hadi 75 desemba 2015 na viti na meza za wanafunzi zimeongezeka kutoka 15, 126 mwaka 2013 hadi 16076 mwaka 2015.

### UJENZI WA MAABARA ZA SAYANSI

Halmashauri ina mikakati ya kuhakikisha kuwa kila shule inakuwa na maabara kwa kila somo la Sayansi (Fizikia, Kemia na Biolojia).Ujenzi wa vyumba hamsini na tisa (59) vya maabara upo katika hatua mbalimbali ili kukamilisha idadi ya vyumba 69 vinavyohitajika. Ambapo hadi tarehe ya leo maabara 59 zimeezekwa na zipo katika hatua ya ukamilishaji.

Mikakati inayoendelea kutekelezwa katika ujenzi na ukamilishaji wa maabara hizo ni pamoja na:-

Halmashauri imetenga kiasi cha Tshs. 130,000,000.00 kwa ajili ya kuimarisha Miundombinu katika idara ya Elimu Sekondari.

## MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO KATIKA ELIMU YA SEKONDARI

- Kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka ili kujenga na kukarabati miundombinu na samani za shule mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa.

- Kuhamasisha wadau mbalimbali wa Elimu ikiwa ni pamoja na jumuiya mbalimbali na mashirika ya umma ili waweze kuchangia utengenezaji wa samani za shule hususani madawati kwa kushirikiana na wananchi, Halmashauri na Serikali Kuu kwa ujumla.

**Mafanikio ya Sekta ya Elimu**:

(i) Ongezeko la uandikishaji wa watoto wanaoanza darasa la kwanza kwa asilimia 134 kwa mwaka 2016 kufikia wanafunzi 9767. Ambapo Wavulana ni 4924 na Wasichana ni 4843

(ii) Kumekuwa na ongezeko la ufaulu wa wanafunzi na kujiunga na Elimu ya Sekondari.

(iii) Kumekuwa na ongezeko la miundombinu ikiwemo madarasa, maabara za sayansi, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na samani katika shule za Sekondari kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano madarasa yaliongezeka kutoka 260 mwaka 2013 hadi 343 Desemba 2016, nyumba za walimu ziliongezeka kutoka 44 mwaka 2012 hadi 75 mwaka 2015 na viti na meza za wanafunzi ziliongezeka kutoka 15,126 mwaka 2013 hadi 16,076 mwaka 2016

**(f) Kuhusu Sekta ya Afya**:

Kwa upande wa Sekta ya Afya, Manispaa imekuwa na mafanikio ya kuridhisha katika uboreshaji na utoaji wa huduma katika Zahanati na Vituo vya Afya. Pia Sekta ya Afya inaendelea na mkakati wa kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Vile vile ujenzi wa hospitali ya Manispaa unaendelea kwa awamu, hadi mwaka 2014 jengo moja la wagonjwa wa nje (OPD) limekamilika.

Katika bajeti ya 2017/2018, Halmashauri iliomba kupitia maombi maalum jumla ya **Tsh2.5billion** kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine mawili kwa ajili ya wodi ya wazazi na jengo la huduma za maabara hata hivyo fedha hizo hazikupatikana. Vivyo hivyo katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri inatarajia kuomba tena ombi maalum la 2.5 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Aidha katika mwaka wa fedha 2017/2018 tunatarajia kuendeleza ujenzi wa kituo cha Afya Sina, Kihonda na Tungi na Zahanati za Kata ya Mbuyuni, Madaganya, Tungi, Konga, Sultan Area, Misongeni, Kibwe na Kauzeni.

### (g) Kuhusu Sekta ya Mazingira na Usafishaji

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Halmashauri iliimarisha shughuli ya usafi wa mazingira kwa kununua magari mawili ya “Skip master”. Vile vile Halmashauri ilitengeneza “skip buckets” 10 katika kuboresha ukusanyaji wa taka ngumu katika maeneo yenye mikusanyiko mikubwa, ili kuongeza kiwango cha uondoaji wa taka ngumu.

Halmashauri inatarajia kununua “skip buckets” nyinge 30 na kuziweka katika Kata mbali mbali. Pia tumenunua vitendea kazi vya usafishaji wa barabara na maeneo ya wazi. Katika utekelezaji wa ushirikishwaji wa jamii, Halmashauri inavyo vikundi vya kijamii 42 ambavyo vinatoa huduma ya ukusanyaji na usafirishaji wa taka ngumu katika Kata. Vikundi hivi vya kijamii vinafanyakazi nzuri ya usafishaji wa mji katika Kata.

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilifanya shughuli za utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na kusimamia matumizi sahihi ya vyanzo vya maji, katika kusimamia matumizi sahihi ya vyanzo vya maji, Halmashauri ilishirikiana na Taasisi ya bonde la Wami/Ruvu kuwaondoa Wananchi ambao wamechukua maji ya mito Ngerengere, Mzinga na mto Morogoro bila vibali.

Pia tulitoa ilani za kisheria kwa Wananchi wanaofanya shughuli za kibinaadamu ndani ya mita sitini katika Kata ya Kauzeni, na Mlimani. Halmashauri ilifanya shughuli ya kuzuia uchafuzi wa mazingira kwa kuwandikia ilani wahusika wa uchafuzi. Pia ukamataji wa wachafuzi wa mazingira ulifanyika ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini na kuwafikisha mahakamani wote waliobainika. Kazi ya kuzuia na kuwaondoa Wananchi wanaojenga, kufyatua tofari, kuchimba mawe na mchanga na kulima katika hifadhi ya vyanzo vya maji inaendelea.

**(h) Kuhusu Sekta ya Maji**:

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina jumla ya mitaa **42** ambayo ipo pembezoni mwa Mji. Mitaa hiyo haijafikiwa na mtandao wa bomba la maji safi na salama kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka (MORUWASA). Kuanzia mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Manispaa ilianza kutoa huduma ya Maji safi na salama katika Mitaa tajwa hapo juu kwa awamu. Mpaka Desemba 2016 jumla ya miradi 13 imetekelezwa katika Mitaa ya Mgambazi, Folkland, Kiswanya, Minazini, Tindigo, Nyambuwa, Bigwa Barabarani na Lukuyu, Lugala,Visole, Kibwe, Kiegea A na Mkoya.

Ujenzi wa miundo mbinu ya Maji inaendelea katika Mitaa ya Kasanga, Misongeni A na B, Tanki la Maji, Bomba la Zambia na Kiegea A ambayo inategemewa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/2016

**Lengo la Manispaa katika usambazaji wa Maji**:

Mwaka 2016/2017, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imekamilisha Mradi wa ujenzi wa maji katika Mtaa wa Kasanga na inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika Mitaa ya Misongeni A na B, Tanki la Maji, Bomba la Zambia na Kiegea A. Pia Ujenzi wa maji katika Mtaa wa Kiegea B upo kwenye hatua ya kumtafuta Mkandarasi wa kukamilisha shughuli zilizobakia mara baada ya kuvunja Mkataba na Mkandarasi wa awali.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Manispaa imelenga kusambaza maji katika Mitaa mitatu itakayokuwa imefanyiwa utatifi na Mtaalam Mshauri katika Kata 12 za pembezoni mwa mji.

**Changamoto katika utekelezaji wa Miradi ya Maji:**

- **Upungufu wa fedha za kutekeleza Miradi:**
  Halmashauri imekuwa ikipokea kiasi kidogo cha fedha ukilinganisha na mipango na Bajeti ya mwaka husika. Hii husababisha Halmashauri kutoweza kutekeleza miradi ya maji kama ilivyopangwa.

- **Kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya Wakazi katika maeneo mbalimbali:**
  Ongezeko la watu katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri hususani kwenye maeneo ya pembezoni mwa Manispaa nayo ni changamoto mojawapo ambayo husababisha miundo mbinu ya maji iliyopo kutokutosheleza katika maeneo hayo.

- **Uvamizi wa vyanzo vya Maji:**
  Kumekuwepo na uvamizi wa vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo na ukataji wa miti kando kando ya vyanzo vya maji na kwenye uoto wa asili, hii husababisha maji kupungua kwa kasi na kusababisha wakazi wa Manispaa kukosa maji hususuani kipindi cha kiangazi. Vile vile ukataji wa miti na uharibifu wa mazingira nao husababisha kuharibu hali ya hewa hivyo kupelekea kukosekana kwa mvua katika vipindi vinavyotarajiwa.

- Upungufu wa Watumishi katika ngazi ya Uhandisi na Ufundi Sanifu

**Mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo:**

Mikakati iliyowekwa ili kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na:

- Kuhakikisha kuwa Halmahsauri inatafuta vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji wakiwemo wahisani, wafadhili, Makampuni na Wadau wa Sekta ya Maji.

- Kutekeleza sheria mbalimbali za mazingira zilizopo ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa

- Kutumia mafundi wa Sekta binafasi
- Kushirikiana na Afisa bonde wa Wami/Ruvu kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu na utunzaji wa vyanzo vya Maji
- Kuhakikisha kuwa maeneo yote yaliyoko pembezoni mwa mji yanapelekewa Miradi ya maji ili kuondoa tatizo la maji katika maeneo hayo.

(i) **Kuhusu Utawala Bora**:

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:
Halmashauri imeendelea na jitihada zake za kuboresha uwezo wa utoaji huduma katika ngazi ya Kata na mpango wa kuendelea kukamilisha ofisi za Kata

Aidha uboreshaji huo uliendelea sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wajumbe wa mabaraza ya usuluhishi ya Kata. Pia Halmashauri inaendelea kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu (MRECOM) na kufanikiwa kusaini mkataba na kampuni ya MAXI MALIPO ambayo itakusanya mapato katika vyanzo vyote vya Halmashauri isipo kuwa chanzo cha uegeshaji wa magari ambacho kinasimamiwa na Halmashauri yenyewe ili kuweza kuongeza mapato kwa lengo la kuzidi kutoa huduma bora kwa wananchi wa Manispaa na hatimaye kuja kufuzu vigezo vya Manispaa kuwa jiji.

Aidha, katika kipindi hiki, Halmashauri imedhamiria kuhakikisha kuwa vikao vyote vya kisheria katika ngazi zote za Halmashauri vinafanyika kwa wakati muafaka na kufuatilia kwa karibu maamuzi yake, na taarifa za fedha zitolewe kwenye ngazi zote.

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:
Katika mwaka 2016/2017, Halmashauri yetu imeweza kufuzu kwa mara nyingine tena vigezo vya Utawala bora hivyo kuweza kuendelea kufuzu kupata fedha za Miradi ya Maendeleo (LGCDG) na ruzuku maalum ya kuboresha miji(ULGSP).

Utawala bora huondoa urasimu usio wa lazima, rushwa , ukiukaji wa Sheria na Taratibu, ukosekanaji wa uwazi, uwajibikaji na migongano isiyo ya lazima kati ya Madiwani na Menejimenti.

Hivyo basi naamini tutaendelea kuwajibika kwa Wananchi wetu kwa kuongeza ushirikiano na uwazi baina yetu na Watendaji kwa maendeleo ya Halmashauri yetu.

### (j) Hali ya maambukizi ya VVU katika Halmashauri kwa kipindi cha Oktoba-Desemba 2016

Katika kipindi cha Oktoba-Disemba 2016 hali ya maambukizi ya VVU ni asilimia **6.6** kwa idadi ya watu waliopima katika vituo mbalimbali ndani ya Halmashauri .katika kipindi cha miezi mitatu Septemba, Oktoba na Novemba .Jumla ya watu **12028** walipima VVU, wanaume **4977** na wanawake **7051** Kati ya watu waliopima, waliopatikana na maambukizi ni **797,** wanaume **270** na wanawake **527.**

Takwimu hizi zinaonesha kuwa kiwango cha maambukizi ya VVU kwa Robo ya pili ya 2016 yamepungua kwa asilimia **0.6** ukilinganisha na kiwango cha maambukizi kwa robo ya kwanza ya 2016, ambapo kiwango cha maambukizi kilikuwa asilimia **7.2** kwa idadi ya watu waliopima.

### (k) Kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato:

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Makisio ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na vyanzo vya Halmashauri yameongezeka kutoka **5,707,408,455.00** kwa mwaka 2016/2017 hadi **6,047,313,187.05** Kwa mwaka 2017/2018 ambapo ni sawa na ongezeko la **shs 339,904,732.05** sawa na **asilimia 5.96**.

**Kuongezeka kwa changamoto za ukusanyaji wa mapato**.

- Utashi mdogo wa walipa kodi katika kutii sheria za kodi.

- Kutokuwa tayari kwa baadhi ya wafanyabiashara wakubwa kulipa kodi kwa hiari

- Kuondolewa kwa kodi ya majengo kwa Halmashauri

**Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato**

- Kupitia upya mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato kwa kuboresha maeneo ambayo yana upungufu.
- Kuwatambua, kuwaorodhesha na kuwapatia namba za utambulisho wamiliki wa majengo yaliyopo ndani ya Manispaa ili waweze kulipa kodi ya majengo.
- Kuendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kukusanya mapato ya Halmashauri kwa mfano Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
- Kuendelea kutoa elimu kwa walipa ili wafahamu umuhimu wa kulipa kodi.
- Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini mianya inayovujisha mapato.
- Kuimarisha mfumo wa kompyuta wa uhifadhi wa kumbukumbu za walipa kodi (MRECOM) na kukusanya mapato kwa njia ya mtandao (E – Cash) kwa kuwatumia Wakala ambao wataanza na vyanzo vinne ambavyo ni Mabango, Kodi za majengo, Masoko na Mapato yatokanayo na huduma za afya (Zahanati na Vituo vya Afya).
- Kuanzisha miradi mipya ambayo Wananchi wanaweza kuchangia ili kuongeza mapato ya Halmashauri.

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:
Bajeti ya Halmashauri ya mwaka 2017/2018 imelenga katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yetu wenyewe na kutumia katika kupunguza kero za Wananchi na kuweka kipaumbele katika utoaji wa huduma za Elimu, Maji, Usafi wa mji, Utawala Bora Afya na Miundombinu.

Ili kutekeleza vipaumbele hivyo Halmashauri inategemea kukusanya/kupokea mapato kutoka vyanzo vya ndani, Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani mbalimbali.

**Mapato ya ndani**

Kwa Mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ilikadiria kukusanya Mapato ya ndani (ownsource) kiasi cha **Tshs 5,707,408,455.00** Hadi kufikia Novemba 2016 Halmashauri iliweza kukusanya kiasi cha **Tshs 2,021,550,455.07** sawa na asilimia **35.42** ya Makisio.

**Ruzuku ya kawaida**:

Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ilikadiria kupokea ruzuku ya matumizi ya kawaida kiasi cha **Tshs 50,486,092,776.00** ambapo mishahara iliyokadiriwa ilikuwa **Tshs.46,387,209,776.00** na matumizi mengineyo yaliyokadiriwa yalikuwa **Tshs 4,098,883,000.00**. Hadi kufikia Novemba, 2016, mapato halisi yaliyopokelewa yalikuwa **Tshs: 19,117,026,100.96** sawa na **asilimia 37.87** ya makadirio, ambapo mishahara ilikuwa **Tshs: 18,281,210,285.96** na matumizi mengineyo **Tshs: 835,815,815.00**

**Ruzuku ya miradi ya Maendeleo**:

Aidha kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ilikadiria kupokea ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani mbalimbali yenye jumla ya **19,445,972,485.20** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, hadi kufikia mwezi Novemba, 2016, Halmashauri iliweza kupokea kiasi cha **Tshs. 7,092,684,851.31** sawa na **asilimia 36.47** ya makisio ya miradi ya maendeleo.

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:

Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Halmashauri inakisia kukusanya/ kupokea mapato kiasi cha **Tshs 84,143,825,944.25** ikiwa ni ongezeko la **Tshs 8,504,352,228.05** sawa ongezeko la asilimia **15** ya makisio ya Mwaka wa fedha 2016/2017 ya Tshs **75,639,473,716.20** kutoka kwenye vyanzo vifuatavyo:

- Halmashauri
- Mapato kutoka Serikali Kuu
- Wahisani

**Makisio ya mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018**:
Katika bajeti ya mwaka 2017/2018, Halmashauri inakisia kukusanya kiasi cha **Tshs. 6,047,313,187.05** kutoka kwenye vyanzo vyake vya Ndani.

Kiasi hiki ni ongezeko la **Tshs. 339,904,732.05** ambayo ni sawa na **asilimia 11.24** ya makadirio ya mwaka 2016/2017 ya Tsh **5,707,408,455.00**

Ongezeko hili litatokana na kuboreshwa kwa ukusanyaji wa mapato ya Ushuru wa Hoteli, Leseni za biashara, kodi ya Huduma (service levy). Adhabu za uvunjaji sheria katika masuala ya usafi wa Mji pamoja na Mauzo ya viwanja.

Katika mapato hayo, jumla ya kiasi cha **Tshs. 3,495,603,625.23** zitatumika kwa ajili ya uchangiaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni sawa na **asilimia 60** ya makisio na **Tshs. 44,128,000.00** zitalipa mishahara kwa watumishi wasiopata ruzuku na matumizi mengineyo ni **Tshs. 2,330,402,416.82** na kiasi cha **Tshs.177,075,145.00** zitatumika katika Vituo vya Afya na Zahanati kupitia mifuko ya utoaji huduma za afya (TIKA,NHIF NA USER FEE).

**Makisio ya mapato ya ruzuku kwa matumizi ya kawaida**:
Kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Halmashauri inakisia kupokea ruzuku ya **Tshs. 59,658,279,588.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya mishahara na matumizi mengineyo, ambapo mishahara inakisiwa kuwa **Tshs. 55,559,396,588.00** na mapato kwa ajili ya matumizi mengineyo yanakisiwa kuwa **Tshs. 4,098,883,000.00**

**Makisio ya mapato ya miradi ya maendeleo**:
Aidha, kwa mwaka 2017/2018 Halmashauri inakisia kupokea ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani mbalimbali ya miradi ya maendeleo kiasi cha Tshs. 18,438,233,169.20 kama ifuatavyo;

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1) | Serikali Kuu | ... | ... | ... | ... | ... | ... | 5,396,668,000.00 |
| 2) | Wahisani (ULGSP) | | ... | ... | ... | ... | ... | 13,041,565,169.20 |
| | **jumla** | **...** | **...** | **...** | **...** | **...** | | **18,438,233,169.00** |

**Kwa mwaka 2017/2018 Manispaa inatarajia kutekeleza Miradi ifuatayo: -**

**Sekta ya Maji**

- Ukarabati wa miundo Mbinu ya maji katika mitaa 3 ya pembezoni itakayokuwa imefanyiwa utafiti na Mtaalamu mshauri.

- Ujenzi wa Miundo Mbinu ya maji katika mitaa 3 ya pembezoni mwa Mji itakayokuwa imefanyiwa utafiti na Mtaalamu mshauri.

**Sekta ya Barabara2017/2018**

- Kufanya matengenezo kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa 2.85 Km. Barabara zitakazohusika ni Msuya, Mafiga, Mgonahazeru, Nunge, Rainbow na Makaburi

- Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Mbete (2.5km), Misongeni – Kingolwira (3.8km), Tubuyu – Tungi (4.7km), Nanasi (1.1km), Sabu (0.8km), Ulanga (0.2km), St. Anna – Kihonda Maghorofani (1.2km), Bondwa Sekondari (1.5km) pamoja na barabara za eneo la Makaburi ya Kola (2.5km).

  - Matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara zenye urefu wa km 499.14km

  - Mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa km 4 barabara za Kichangani na Ipo ipo- Kihonda Maghorofani.

## (g) Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

- Kujenga kituo cha kusindika na kufungashia mazao ya nyanya katika kata ya Kihonda Maghorofani.
- Kuanzisha shamba la mfano la kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya matone katika kata ya Tungi
- Kuanzisha vyama vya ushirika vya masoko ya mazao ya kilimo katika kata za Luhungo, Bigwa na Kauzeni.
- Kuanzisha mashamba darasa 4 ya usindikaji wa mboga na lishe kwa Wakina mama katika kata za Kihonda Maghorofani , Kauzeni na Tungi.
- Kuanzisha mashamba darasa 5 ya zao la nyanya kwa vijana katika kata za Luhungo, Kauzeni, Mkundi, Bigwa na Kihonda
- Kujenga machinjio 1 ya nguruwe katika kata ya Mazimbu
- Kujengea uwezo wasindikaji wa zao la ngozi katika Manispaa

## Sekta ya Elimu Msingi

- Kujenga Matundu 24 ya vyoo katika Shule ya Msingi za Mbuyuni,Mkundi,Azimio na Bigwa na kuchangia ujenzi wa matundu 16 ya vyoo katika Shule za Kilongo,Kikundi, Mkwajuni,Mwere A na B
- Kujenga vyumba vitatu vya madarasa katika Shule za Bungo,Kihonda, na Kauzeni kwa ajili ya Watoto wenye Ulemavu.
- Kuchangia ujenzi wa vyumba 14 vya madarasa katika Shule za Msingi za Manispaa
- Kumalizia ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu katika Shule ya Msingi Mbuyuni na kuchangia ujenzi wa nyumba moja katika Shule ya Msingi Ujirani
- Kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Walimu katika Shule ya Msingi Mazimbu A
- Kujenga vyumba vya madarasa viwili katika Shule ya Msingi Kilongo

- Kukamilisha ujenzi wa Vyumba vya Madarasa 20 katika Shule za Mkwajuni,Azimio,Bigwa,Ujirani,Kilongo,Msamvu B , Lukobe na Shule tarajiwa za Mawasilano na Lugala.

**Sekta ya Sekondari**

- Kusaidia ujenzi wa matundu ya vyoo 27 katika shule za Sekondari.
- Uendelezaji wa Ujenzi wa maabara katika shule za sekondari 21.
- Majego mawili ya utawala yatakamilishwa katika shule ya sekondari za Mgulasi na SUA

**Sekta ya Afya**

- Ukamilishaji wa Kituo cha Afya SINA, na Misongeni
- Ujenzi wa zahanati za, Mbuyuni, Sultani Area, Kibwe, Konga, Tungi, Kauzeni na Kiwanja cha Ndege
- Uendelezaji wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.
- Ujenzi wa chumba cha upasuaji kituo cha Afya Mafiga
- Ujenzi wa shimo la kutumia kondo la nyuma "Placenter Pits" katika Zahanati za Kichangani na Mji Mpya.
- Kuendelea kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya Vituo 21 vya kutolea huduma za Afya vinavyomilikiwa na Halmashauri.

**Sekta ya Mazingira na Usafirshaji**

- Ukarabati wa mabwawa ya viwandani katika Kata ya Mafisa maarufu kwa jina la TLAI.
- Kuboresha dampo lililoko katika Kata ya Mafisa kwa kukodi mitambo ya "Excavator" na "Bulldozer" ili kuchimba mashimo na kuzifukia taka kwa kiwango kinachotakiwa kisheria.

**Sekta ya Mipangomiji**

- Kufanya upimaji wa viwanja 500 katika maeneo ya Mkundi, Kiegeya, Kingolwira, Madanganya, Mindu, Chamwino, Mji Mpya, Bigwa na Kihonda ifikapo Juni, 2017
- Kufanya uthamini wa ekari 50 pamoja na ulipaji wa fidia,

- Kuendelea kuhamasisha wananchi ulipaji wa kodi ya pango la ardhi hadi kufikia lengo la Tshs. 1,400,000,000/= kwa mwaka; kama yalivyo maelekezo ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendelo ya Makazi kwa Halmashauri yetu; na
- Kuandaa Hati miliki 2,500 ifikapo Juni, 2017

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi**:
Tunayo haki ya kujipongeza, pamoja na kujipongeza bado tuna changamoto kubwa ya kufanya vizuri zaidi, hivyo ninawaomba wote kwa ujumla kuimarisha ushirikiano na kila mmoja kutimiza wajibu wake wa kulipa kodi inayostahili na kwa wakati muafaka ili kukusanya kiasi tulichojiwekea.

Kufanya hivyo kutaiwezesha Halmashauri yetu kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kutoa huduma bora kwa Wananchi wake.

Pamoja na changamoto zilizo mbele yetu, ninapenda kumalizia kwa kusisitiza kwamba katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 mambo makuu saba yafuatayo yataendelea kupewa kipaumbele:

i) Mapato,
ii) Usafi wa Mji,
iii) Utawala bora,
iv) Elimu,
v) Miundombinu,
vi) Afya na;
vii) Maji

Aidha, uongozi uhakikishe kuwepo kwa uwajibikaji katika ngazi zote na kwa nguvu zote.

**Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:**
Nashukuru kwa kunisikiliza na napenda kutamka kuwa Mkutano huu nimeufungua rasmi, ewe Mwenyezi Mungu tusaidie.

……………………………………
*Mhe. Pascal Kihanga,*
**MEYA WA MANISPAA,**
**MOROGORO**